TANGAZO LA SERIKALI Na. 513 la Tarehe 14/9/2018

SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa Chini ya Kifungu Cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA ZA VIBALI VYA BURUDANI) ZA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada za vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Mji Kondoa na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Halmashauri ya Mji Kondoa.

Tafsiri

3. *"Ada"* maana yake ni kiwango cha fedha kitakachopangwa na Halmashauri na kutozwa katika shughuli za Burudani yoyote isipokuwa ile ya kiserikali au madhehebu ya kidini;

*"Afisa Mwidhiniwa* maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*"Halmashauri"* maana yake ni Halmashauri ya Mji Kondoa;

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

*"Burudani"* maana yake ni tukio ambalo litakuwa linafanyika kwa kukusanya watu mbalimbali katika ukumbi au eneo lolote litakalo ruhusiwa na Halmashauri;

*"Sherehe"* ina maanisha ni tukio la mkusanyiko wa watu zaidi ya watu ishirini na kufanyika katika ukumbi, mtaa, uwanja au eneo lolote litakaloruhusiwa na Halmashauri;

*"Ukumbi wa video"* maana yake ni jengo lolote lililoidhinishwa na Halmashauri kwa shughuli za kuonesha video;

*"Video na Sinema"* maana yake ni picha zozote zinazooneshwa katika kumbi za video na sinema na zenye maadili mema;

Kibali

4. (1) Kila mtu au taasisi yeyote isiyokuwa ya kiserikali au kidini itakayoendesha shughuli za burudani, atalazimika kuomba kibali cha kuendesha shughuli hiyo toka Halmashauri kama kilivyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kibali hicho kitalipiwa ada kama itakavyoonyeshwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(3) Kibali hicho kitaonesha;-

(a) sehemu itakayofanyika shughuli hiyo.

(b) muda wa kuanza na kumalizika kwa shughuli hiyo.

(c) aina ya Shughuli au burudani

(4) Nakala ya kibali hicho itapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) ikiwa na viambatanisho vyote husika.

Marufuku

5. (1) Ni marufuku kwa mwenye ukumbi wa Video na Sinema au sehemu yoyote kuonyesha picha za video ambazo hazina maadili ikiwa ni pamoja na zile zinazoonyesha ngono na ujambazi.

(2) Ni marufuku kwa wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane (18) kuingia katika kumbi za burudani au muziki.

Wajibu

6. (1) Ni wa jibu wa kila mmiliki wa ukumbi wa muziki kupiga muziki kwa kiwango cha sauti cha kawaida bila kuathiri watu wanaozunguka eneo la ukumbi huo wa mziki.

(2) Kila mwonesha video au sinema atatakiwa kuweka sauti ya chini wakati wa onesho bila kuathiri majirani wanaomzunguka.

(3) Ni wajibu wa kila mmiliki wa kumbi za burudani au bar au mziki kuhakikisha wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri

wa miaka kumi na nane (18) aingii katika kumbi izo na endapo itabainika kuingia kwa wanafunzi/watoto hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mmiliki wa kumbi hizo.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

7. Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika ukumbi wowote wa burudani, sinema au sherehe yeyote inayofanyika mtaani na hadharani kukagua kibali kinachoruhusu uendeshaji wa shughuli hiyo.

Kibali Maalum

8. Mtu au kikundi chochote kitakachofanya sherehe katika mitaa itabidi apate kibali cha kufunga barabara ya mtaa.

Muda wa Burudani

9. (1) Muda wa kuonesha video au sinema utakua ni siku ya jumamosi na jumapili kuanzia saa saba mchana hadi saa kumi na mbili jioni.

(2) Disco litaruhusiwa kupigwa siku ya ijumaa hadi jumapili kuanzia saa tatu usiku hadi saa tisa usiku.

Wajibu kwa Halmashauri wa kulipa fidia

10. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kulipa fidia ya hasara itakayosababishwa na Afisa Mwidhiniwa au Afisa yeyote kwa uzembe au makusudi wakati wa kukusanya Ada na Ushuru au wakati anatekeleza Sheria Ndogo za Halmashauri.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyochopungua shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (Tshs. 500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama itakavyoelekezwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) jela na kisichozidi miaka miwili (2) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo..

JEDWALI LA KWANZA

*Limetungwa Chini ya kifungu cha 4 (1)*

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI

SEHEMU YA KWANZA (Taarifa za Mwombaji)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mwombaji au Kampuni;<br>.......................................... | 2. Anwani ya Mwombaji;<br>.......................................... |
| 3. Aina ya Shughuli;<br>.............................. | 4. Eneo analokusudia kufanya shughuli<br>.......................................... |

| | |
|---|---|
| 5. Muda wa kuanza ; ......................................... | 6. Muda wa kumaliza ................................... |
| 7. Ada ya kibali Tsh. ................................ | 8. Stakabadhi ya malipo; ................................... |
| Saini: ............................................. Tarehe: ........................................... | |

SEHEMU YA PILI (Kwa Matumizi ya Ofisi)

| | |
|---|---|
| 1. Maombi Na.................................. | 2. Ada ya kibali Sh:. ........................ |
| 3. Namba ya Stakabadhi ya malipo: ........... | 4. Tarehe:................................... |

Maoni ya Afisa Mwidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali (*weka alama ya tiki kwa inayohusika*)

Sababu:

..................................................................................................

Jina: .................................................... Saini:.......................

Tarehe: ............. Mwezi...................... Mwaka................

JEDWALI LA PILI

*Limetungwa Chini ya Kifungu cha 4(2)*

ADA ZA SHUGHULI ZA BURUDANI

| Na. | Aina ya Shughuli | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Muziki wa dansi kutoka nje ya Halmashauri | Tsh 50,000/= |
| 2. | Muziki wa dansi wa ndani ya Halmashauri | Tsh 30,000/= |
| 3. | Muziki wa disco | Tsh 20,000/= |
| 4. | Promotion- Makampuni | Tsh 30,000/= |
| 5. | Shindano la mpira | Tsh 10,000/= |
| 6. | Maonesho ya Sinema na Video | Tsh 15,000/= |
| 7. | Kufunga barabara ya mtaa | Tsh 10,000/= |
| 8. | Shindano la kutafuta msanii au urembo au mavazi | Tsh 50,000/= |

JEDWALI LA TATU
*(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 11)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........................................................................... nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya........................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa kwamba mnamo tarehe ......... ya Mwezi................. Mwaka ............ nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ........ cha Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Mji Kondoa za Mwaka 2018

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe ..................... Mwezi .......................Mwaka...............

Jina: ..........................................................................................

Saini: ..........................................................................................

Mbele ya: ..........................................................................

Cheo: ..........................................................................................

Saini: ..........................................................................................

Tarehe: ..........................................................................................

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa kondoa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 13/5/2017 mbele ya:-

KHALIFA KONDO
*Mkurugenzi wa Mji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

L.S

HAMZA MAFITA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

NAKUBALI,

DODOMA,
15 Agosti, 2018

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*